KWA JINA LA ALLAAH, MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

# Al-Hudaa [Uongofu]

# الهدى

Volume 13, Issue 1

5th Ramadhân 1432

5th Aug, 2011

YALIYOMO

SUNNAH ZA RAMA... 1 - 3

KUFUNGUA SAUM 3 - 4

## SUNNAH ZA RAMADHAAN ZILIZOSAHAULIWA

**Na Sheikh Muhammad Naasirud-Deen aL-Albaani (رحمه الله)**

Na Imaam Muhammad Nassir ud-Deen al-Albanee (rahimahullah)

Lakini leo, sisi tunateleza kwenye makosa mawili:
1) Kosa la kwanza, tunaucheleweshe muadhini kupita wakati uliopangwa kisheria. Kisha baada ya ucheleweshaji huo, kuna ucheleweshaji mwengine, nao ni, tunakaa kitako kwa maandalizi ya chakula- isipokuwa watu wachache wenye bidii wanaokwenda kuswali swala ya Magharibi msikitini. Lakini idadi kubwa ya watu husubiri mpaka wasikie muadhini, kisha wakae kitako waandae chakula utadhani ndio wanakula chakula cha usiku, na sio kufungua saumu zao tu.
Miadhini yenyewe siku hizi- kwenye sehemu nyingi sana za miji ya waislamu, kwa bahati mbaya inanibidi

JIPATIE KITABU CHA

**“SAUMU YA MWEZI WA RAMADHÂN KAMA ILIVYOTEKELEZWA NA MTUME (صلى الله عليه وسلم).”**

TUPIGIE SIMU KATIKA NAMBA HIZI:

+254- 0721473181 AU

+254-0727341779




niseme, na sio mjini Jordan peke yake, na nayajua mambo haya baada ya kuyafanyia uchunguzi, katika sehemu nyingi za miji ya kiislamu- Miadhini ya Magharibi huadhiniwa baada ya wakati wake kupita. Na sababu ni kwamba tumeacha kujiambatanisha na utekelezaji wa sheria ya kiislamu, na badala yake tumejitegemeza na hisabu za utaalamu wa ilimu ya nyota. Tunategemea orodha za nyakati (Timetable).
Orodha hizi za nyakati zime-egemezwa juu ya hisabu za utaalamu wa ilimu ya nyota ambazo zinahesabu ardhi kuwa ni sehemu moja isiyoinuka wala kushuka (iliyotandazika). Wameukisia wakati kulingana na hiyo sehemu, ambapo ukweli ni kwamba ardhi yoyote hususan katika hii ardhi yetu hubadilika. Hubadilika baina ya kuzama kwa mabonde na kuinuka kwa milima. Kwahivyo ni makosa kutoa wakati mmoja ukaenea ufuoni, barani na milimani. Hapana! kila sehemu ya ardhi ina wakati wake na mtu yeyote mwenye uwezo katika sehemu yake ya makaazi, kwenye mji au kijijini mwake akaweza kulishuhudia jua likitwa kwa macho yake mwenyewe, basi huo ndio uharakishaji tulioamrishwa katika maneno yake (صلى الله عليه وسلم) tulokwisha yataja hapo awali: "Umma wangu wataendelea kudumu katika kheri, maadamu wao watakuwa ni wenye kuharakisha kufungua saumu (futari)..." . Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa na tahadhari mno katika kuitekeleza Sunnah hii kwa kuifundisha na kuifanya yeye mwenyewe. Kuhusu mafundisho yake, amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم) katika Hadeeth iliyopokewa na Imaam al-Bukhari katika saheeh yake (no.1954): "Usiku ukijitokeza upande huu," na akaashiria upande wa sehemu ya mashariki, "Na mchana ukawa umeshaondoka kutoka huku," na akaashiria upande wa sehemu ya magharibi, "Na jua limeshakutwa- basi saumu ya aliefunga inamalizika".
Ni nini maana ya 'Saumu ya aliefunga inamalizika?', Ina maana yakwamba ameingia chini ya hukmu ya kufungua saumu yake. Kisha hapo inakuja ile hukmu iliyopita ambayo Mtume (صلى الله عليه وسلم), alipohimiza kufungua saumu. Hilo ni jambo ambalo alilokuwa akilitekeleza hata kama alikuwa juu ya kipando chake (Ngamia) akiwa safarini. Akapokea Imaam al-Bukhari (Hadeeth no.1955) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimuamrisha mmoja wa Maswahaba zake amtayarishie Iftaar (kitu cha kufungua saumu), Nae yule Swahaba akamjibu, 'Ewe Mtume wa Allaah, bado tuko katika mchana'. Ikiwa na maana yakwamba muangaza wa jua ungali uking'ara upande wa magharibi ingawa jua lenyewe lilikuwa limeshakutwa. Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakumuitikia alivyosema, bali aliendelea kumsisitiza amtayarishie Iftaar. Hapa mpokezi wa Hadeeth hiyo akasema, 'Muangaza wa mchana ulikuwa umetukabili', [maana yake: muangaza wa mchana, muangaza wa jua). Tulipofungua saumu zetu, akasema, 'Lau mmoja wetu angelipanda juu ya Ngamia, angeliliona jua'. Huu ndio wakati jua lilipokutwa na Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamuamrisha mmoja wa Maswahaba zake amtayarishie Iftaar. Kwa nini? kuharakisha juu ya jambo la kheri:"Umma wangu wataendelea kudumu katika kheri, maadamu wao watakuwa ni wenye kuharakisha kufungua saumu (futari)... ".
Jambo la muhimu hapa ni kwamba, tumeshaona vile Iftaar ilivyoshurutishwa kuharakishwa kisheria ambayo ni lazima ifanywe kwa kutumia tende chache. Kisha ni lazima tuharakishe kuswali swala ya

*(Endelea kwenye Ukurasa wa 2)*

*(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)*

Magharibi na baadae watu wanaweza kukaa na kula- shibe yao. Hili ndilo jambo la kwanza nililokusudia kuwakumbusha na jinsi ya kuyapatanisha mas-ala hayo mawili ambayo Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliyotuamrisha kuyatekeleza kwa haraka. La kwanza ni amri ya kuharakisha kufungua saumu, na la pili ni amri ya kuharakisha kuitekeleza swala ya Magharibi. Kwahivyo Iftaar na itekelezwe na tende kiasi, kama ilivyo katika Sunnah, na ikiwa hazikupatikana tende, basi kwa tama la maji. Kisha swala nayo na iswaliwe kwa jama'ah msikitini.

2) Mas-ala mengine nipendayo kuyakumbusha ni hayo yaliotokea katika hadeeth hizo zilizopita: "...Na kucheleweshe daku (suhoor)". Maana yake: kinachohitajika hapa ni kinyume cha hali hiyo ya Iftaar. Akatuamrisha sisi Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuharakisha kula Iftaar. Lakini kuhusu suhoor, basi icheleweshwe. Mambo yalivyo siku hizi ni kinyume kabisa na hivyo, kwani watu wengi hula suhoor kabla ya kutokeza kwa Alfajiri kwa kiasi cha muda wa saa nzima. Hii haifai. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sunnah iliyofunzwa na Hadeeth za Mtume (صلى الله عليه وسلم) na mafundisho yake. Maswahaba wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) walikuwa wakichelewesha suhoor sana, kiasi cha kwamba mmoja wao hufikilia kuusikia muadhini hali yakuwa bado anakula. Alikuwa akichelewesha suhoor.

Kwa hakika kuna Hadeeth iliyo saheeh iliyopokelewa kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) inayo-onyesha urahisi ulioekwa na Uislamu ambao unafaa kutambuliwa kama ni miongoni mwa misingi ya Uislamu ambayo waislamu wanayojivunia nayo. Nayo si mengine bali ni mas-ala ya kufunga, kwani Allaah (سبحانه وتعالى) ameimalizia aya inayohusiana na kufunga kwa kusema: (kama ilivyofasiriwa) "AllaahAnakutakieni yalio mepesi wala hakutakieni yalio mazito." (Surah al-Baqarah 2:185) Ni kutokamana na wepesi huu ndipo akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم):

"Atakaposikia muadhini mmoja wenu (na huku) akawa ameshikilia chombo mikononi mwake, basi na asikiweke chini (chombo hicho) mpaka amalize hamu yake."

'Atakaposikia muadhini mmoja wenu (na huku) akawa ameshikilia chombo', Hicho ni chombo chenye chakula, emma iwe ni maziwa, kinywaji, maji au kitu chochote ambacho mtu atakuwa anakula kama suhoor. Atakaposikia muadhini, basi na asiseme, 'Sasa chakula kimeshakuwa ni haraam na haifai kula chochote mfano wa maziwa, au matunda au chochote nilichobakisha'. Lakini ukweli ni kwamba kwa yule atakaeusikia muadhini na akawa bado hajajitosheleza na mahitaji yake kutoka katika chakula na kinywaji, basi Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamuhalalishia. Na akasema waziwazi, kwa lugha ya kiarabu iliyo fasaha: "Atakaposikia muadhini mmoja wenu (na huku) akawa ameshikilia chombo mikononi mwake, basi na asikiweke chini (chombo hicho) mpaka amalize hamu yake."

Na maana ya muadhini hapa ni muadhini wa pili, sio muadhini wa kwanza, wanaouita al-Imsaak (muadhini wa kujizuia). Inatupasa kujua yakwamba muadhini huo (muadhini wa kujizuia au muadhini wa kwanza), hauna ushahidi wowote katika sharia. Muadhini wa pili ndio wakati tunapotakikana kujizuia, na ushahidi wake ni kutoka katika Qur'aan Aliposema Allaah (سبحانه وتعالى) (kama ilivyofasiriwa): "Na kuleni na kunyweni mpaka ubainike kwenu weupe wa Alfajiri katika weusi wa usiku."(Surah al-Baqarah 2:187) Hapo unapoanza wakati wa swala ya Alfajiri ndipo inapokuwa kula ni haraam. Hapana tafauti yoyote baina ya mambo hayo mawili. Hakuna kujizuia kula au kunywa kwa robo saa au chini ya hapo au zaidi ya hapo kabla ya kuanza kwa wakati wa swala ya Alfajiri. Hakuna kabisa!

Kwa vile inapasa kuswaliwa Alfajiri kunapopambazuka, basi na chakula nacho kinakuwa ni haraam kwa mwenye kufunga kunapopambazuka. Kwahivyo hakuna tafauti yoyote baina ya mambo hayo mawili kabisa. Utaona katika hadeeth ambayo Imaam al-Bukhari na Imaam Muslim wameafikiana kwayo, iliyopokewa na 'Abdullah ibn 'Umar ibn al-Khattaab (رضي الله عنهما) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "Musidanganyike kwa muadhini wa Bilaal."Maana yake: muadhini wa kwanza,"Kwa sababu yeye huadhini kwa kumuamsha mtu alielala ili atakae kula suhoor aamke apate kula. Kwahivyo, kuleni na kunyweni mpaka ibn Umm Maktum aadhini." Ibn Umm Maktum, jina lake ni 'Amr, alikuwa ni kipofu. Nae ndie yule ambae aliehusika katika maneno ya Allaah(سبحانه وتعالى) kama ilivyofasiriwa): "Alikunja (Mtume) paji na akageuza uso, kwa sababu alimjia kipofu." (Surat 'Abasa 80:1-10) Huyu ndie aliekuwa akiadhini muadhini wa pili, ambao ni wenye kumaanisha yakwamba wakati huo, kula inakuwa ni haraam na umeingia wakati wa swala ya Alfajiri.

*(Endelea Kwenye Ukurasa wa 3)*

## TANGAZO LA DARSA ZA RAMADHÂN 2011/1432H

**MASJID MAZRUI** [KILA SIKU BA'DA SWALAAT ADH-DHUHR]

JUMATATU HADI JUMATANO / [Nawaaqidh ul-Islaam] / Ustadh Athman Bin Na'man

ALKHAMIS / [-] / Ustadh Sharrif

JUMAMOSI NA JUMAPILI / [AL-WAABIL AS-SWAYYIB] / Abu 'Abdur-Razzaq Haruna Rass.

**DARSA ZA WANAWAKE MASJID MAZRUI NI KILA SIKU [ISIPOKUWA IJUMAA] KUANZIA SAA NNE ASUBUHI MPAKA SAA SITA.**

**MASJID KHAYRAAT [KIZIWI]** [BA'DA SWALAAT ADH-DHUHR]

JUMANNE NA ALKHAMIS / [Ustaadh Muhammad Abdillah]

JUMATANO / [TAS-HEEL AL-AQEEDAH] / Abu Abdur-Razzaq Haruna Rass.

**Unaweza kusikiliza Darsa hizi kwenye Mtandao (Internet)**

Pal-Talk ⟹ All-Rooms ⟹ Religion & Spirituality ⟹ Islam ⟹ Callers to Tawheed ⟹ Swahili Duroos.

*(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)*

Ni vipi mtu huyu alikuwa akiadhini haliyakuwa alikuwa ni kipofu? Hapana shaka suala hili humjia mtu yoyote. 'Amr ibn Umm Maktum alikuwa akipanda juu ya sakafu ya msikiti na alikuwa haoni kiangaza cha asubuhi kunapopambazuka, lakini alikuwa akingoja mpaka watu watakapompa ishara. Watakapo-ona watu yakwamba kiangaza kimeanza kujitokeza na kusambaa katika upeo wa macho, ndipo watakapoanza kumwambia, 'Sasa ni Asubuhi, sasa ni Asubuhi'. Kisha nae aanze kuadhini. Muadhini huu wa 'Amr ibn Umm Maktum ulikuwa ni baada ya kuingia Alfajiri, na kushuhudiwa na watu wanaotembea njiani. Na alipoambiwa 'Sasa ni Asubuhi, sasa ni Asubuhi', ndipo yeye anapoadhini. Kwahivyo katika jambo hili kuna nafasi ya ruhusa, kwani mwenye kuadhini huchelewesha kuadhini mpaka atakapowasikia watu wakimwambia, 'Sasa ni Asubuhi, sasa ni Asubuhi'. Kisha isitoshe, Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "Atakaposikia muadhini mmoja wenu (na huku) akawa ameshikilia chombo mikononi mwake, basi na asikiweke chini (chombo hicho) mpaka amalize hamu yake." Allaah (سبحانه وتعالى) Amesema kweli Aliposema mwishoni mwa zile aya zenye kuhusiana na kufunga (kama ilivyofasiriwa): "Allaah Anakutakieni yalio mepesi wala hakutakieni yalio mazito"

Na Akaendelea kusema (kama ilivyofasiriwa): "Na pia (Anakutakieni) mtimize hisabu hiyo, na (Anakutakieni) kumtukuza Allaahkwa kuwa Amekuongozeni, ili mpate kumshukuru." Ni miongoni mwa mafunzo ya Fiqh yanayostahiki kupingwa na yanayokwenda kinyume na Sunnah pale anaposema mtu, 'Mtu anaposikia muadhini na akawa na chakula mdomoni mwake, itambidi akiteme (chakula hicho)'. Huku ni kupita kiasi na kupindukia mipaka katika dini (ghuluww). Allaah (سبحانه وتعالى) Mola wa walimwengu wote, Ametukemea na kutukumbusha katika kitabu chake na katika Sunnah za Mtume wake (صلى الله عليه وسلم) yakwamba tusipindukie mipaka kwenye dini yetu. Akasema katika Qur'aan (kama ilivyofasiriwa): "Enyi watu wa kitabu! Msipindukie mipaka katika dini yenu, wala msiseme juu ya Allaahila yaliyo kweli."(Surat An-Nisaa 4:171). Na Mtume wetu (صلى الله عليه وسلم) ametwambia au amesema: "Jitahadharini na kupindukia mipaka katika dini (ghuluww), kwa sababu wale walokuja kabla yenu waliangamizwa kwa ajili ya kupindukia mipaka katika dini zao" Kwahivyo ikiwa Mtume wa Allaah (صلى الله عليه وسلم) ashatwambia waziwazi yakwamba mtu anapokula daku (suhoor), kuna nafasi ya ruhusa na kipengee cha usahali mpaka akafikilia kiwango cha kusema: "Atakaposikia muadhini mmoja wenu (na huku) akawa ameshikilia chombo mikononi mwake, basi na asikiweke chini (chombo hicho) mpaka amalize hamu yake." Mtu yoyote mwenye kusema 'Atakaesikia muadhini na akawa na chakula mdomoni mwake ni lazima akiteme', ajue yakwamba anapingana na Allaahna Mtume wake (صلى الله عليه وسلم). Hiyo si katika Sunnah, bali huko ni kwenda kinyume na Sunnah na ni kinyume cha maamrisho yalio wazi ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) Na nimeshawahi kuulizwa mara nyingi sana, kwahivyo sitoyaacha yale yanayohitajiwa kwenye suala hilo. Mimi nitawatangulia kwa kusema yakuwa Hadeeth hii inapatikana katika vitabu mashuhuri vya Sunnah kama vile Sunan Aboo Dawud ambacho ni kitabu cha tatu katika orodha ya vitabu sita vyenye kutambulika zaidi. Cha kwanza ni Saheehul-Bukhari, cha pili ni Saheeh Muslim na cha tatu ni Sunan Aboo Dawud. Hadeeth hii inapatikana kwenye kitabu hicho. Na vilevile imepokewa na Aboo 'Abdullah al-Haakim katika kitabu chake kiitwacho Mustadrak na pia imepokewa na Imaam, Imaam wa Sunnah Ahmad ibn Hanbal (رحمه الله) kwenye kitabu chake mashuhuri kiitwacho Musnad Imaam Ahmad. Hadeeth hiyo si hadeeth geni, bali ni hadeeth mashuhuri sana na imepokewa na ma-Imaam wa Sunnah wa zamani kwa riwaya zenye upokezi ulio saheeh. Basi mpaka hapa namalizia mazungumzo yangu na pengine wengine wenu muna maswali ambayo tutajaribu kuyajibu Allaah Akituwezesha. Namalizia kwa maneno yake (صلى الله عليه وسلم) "AllaahAnapenda mno ruhusa Yake itekelezwe kama vile Anavyopenda amri Zake zitekelezwe",na kwenye riwaya nyengine,"Kama ambavyo anavyochukia Anapofanyiwa ma'asia.

Hapa pana riwaya mbili, 'Allaah Anapenda mno ruhusa Yake itekelezwe kama vile Anavyopenda amri Zake zitekelezwe' na kwenye riwaya nyengine, 'Kama ambavyo anavyochukia Anapofanyiwa ma'asia.

Basi Muislamu hafai kuwa mcha Mungu wa kirongo, na (matokeo yake) akawa mbali na kumtwi'i Mtume (صلى الله عليه وسلم), katika yale aliyotuhimiza kushikamana nayo na kutufafanulia. Na nilioyasema yanatosha, na sifa zote njema ni za Allaah, Mola wa viumbe vyote.

## KUFUNGUA SAUMU (*Iftwâr*)

Na: Sheikh Ali al-Halabi na Salim al-Hilaalee

### Ni Wakati Gani Mwenye Kufunga Anapofungua Saumu Yake?

Amesema Allâh (سبحانه وتعالى): **"Kisha timizeni Saumu mpaka usiku."** Mtume akaifafanua kumaanisha kuingia kwa usiku na kuondoka kwa mchana na kupotea kwa mviringo wa jua. Tumeshanukuu ya kutosha ili moyo wa Muislamu anayefuata Sunnah upate kutulia. Basi Ewe mja wa Allâh, unayo maneno ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) mbele yako na ushayasoma, na hali alivyokuwa akifunga si zenye kufichika kwako, na umeshaona vitendo vya Maswahaba zake (رضي الله عنهم)– nao walikuwa wakiandama kwa tahadhari, hatua kwa hatua kila alichokileta Mtume wa kuigwa. Kutoka kwa 'Amr Ibn Maimoon al-Awdee aliyesema: "Maswahaba wa Muhammad (صلى الله عليه وسلم) ndiwo waliokuwa wa mapema zaidi miongoni mwa watu katika kuanza kufungua saumu (*Iftwâr*) na ni wa mwisho kabisa katika kula daku (*suhoor*).

### Kuharakisha Kufungua Saumu

Basi, Ewe ndugu katika Imaan, unatakiwa kufungua saumu yako pindi tu pale jua linapokutwa na wala usibabaishwe na muangaza mwekundu unaobakia katika anga. Katika kufanya hivyo, utakuwa unafuata Sunnah za Mtume wako (صلى الله عليه وسلم) na kujitafautisha na Mayahudi na Manaswara kwani wao huchelewa kufungua saumu zao mpaka nyota zianze kujitokeza. Kuifuata njia ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) na kuihudumikia Sunnah yake inamaanisha kudhihirisha alama za kuiashiriya dini zimeinuliwa juu, na kwamba tunajivunia na uongofu ambao tuko juu yake – na tukitarajia yakwamba sote (Binadamu na Majini) tutajumuika juu ya hilo. Na yanabainisha haya, ahaadeeth za Mtume (صلى الله عليه وسلم) katika ibara zifuatazo:

### Kuharakisha Kufungua Saumu Huleta Kheri

Kutoka kwa Sahl Ibn Sa'd (رضي الله عنه) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "*Watu hawatoacha kuwa katika kheri maadamu wataharakisha*

*(Endelea Kutoka Ukurasa wa 3)*

*kufuturu.*"

**Kuharakisha Kufungua Saumu Ni Sunnah Ya Mtume (صلى الله عليه وسلم)**

Pindi Ummah wa Ki-Islamu utakapoharakisha kufungua saumu basi utakuwa umebaki juu ya Sunnah ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) na njia ya watu wema waliotutangulia na wala hawatopotea, kwa idhini ya Allâh, maadamu watakuwa wameshikamana vilivyo na hayo (Sunnah za Mtume (صلى الله عليه وسلم) na kukataa chochote chenye kuipinga (Sunnah) hiyo.

Kutoka kwa Sahl Ibn Sa'd (رضي الله عنه) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Ummah wangu hautoacha kuwa juu ya Sunnah zangu maadamu hawazingoji nyota pindi wanapofungua saumu zao."*

**Kuharakisha Kufungua Saumu Ni Katika Kuwakhalifu Waliopotea Na Walioghadhibikiwa**

Iwapo watu wataendelea kuwa katika kheri kwa sababu wanafuata njia ya Mtume wao na wakashikamana na Sunnah zake basi Uislamu utabaki kuwa juu na utashinda na wala hautodhuriwa na wenye kuupinga. Kisha Ummah wa ki-Islamu utakuwa ni taa inayong'ara kwenye giza zito, na mfano mzuri wa kuigwa kwa sababu hautokuwa ni mkiya wa Mataifa ya Mashariki wala Magharibi, wala ngao ya kila apigae mayowe (makelele), mwenye kupinda anapovumishwa na upepo kuelekea mahali popote pawapo. Abu Hurairah (رضي الله عنه) amesema yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Dini haitowacha kushinda maadamu watu watakuwa ni wenye kuharakisha kufungua saumu, kwani Mayahudi na Manswara huchelewesha."*

Twasema sisi katika ahaadeeth ambazo tulizozisoma sasa hivi yakwamba ndani yake muna faida nyingi zilizobainishwa kama zifuatazo:

Yakwamba dini itakayobakia kudhihiri na bendera yake ikipepea juu itategemea juu ya kufanya mambo yaliyo kinyume cha Mataifa yaliyopita waliopewa kitabu. Kuna mafunzo katika haya kwa Waislamu yakwamba watajipatia kheri katika kila kitu ikiwa watabaki kuwa ni wenye kutambulika juu ya uongofu – bila ya kulemea sehemu za Mashariki wala Magharibi; wakiwa ni wenye kukataa kuwa ni vibaraka vya Warusi au wenye kuparuza juu ya nyasi kavu za mabustani ya Nyumba-Nyeupe (White-House), twamuomba Allâh aipige weusi nyumba hiyo, wala wasigeuze nyuso zao na kuelekea London, twamuomba Allâh auteketeze mji huo na auvurumizie jaani. Kwa sababu ikiwa watafanya hivi (kuwakhalifu Mataifa yaliyotangulia) basi watasimama mbele ya halaiki ya Mataifa wakitizamwa kwa heshima na ta'adhima kubwa na nyoyo zitakuwa ni zenye kuwapenda wao – lakini hayo hayatotokea isipokuwa kwa kuregea kwenye Uislamu unaopatikana kwenye Kitaab na Sunnah, katika 'Aqeedah (Imani) na Manhaj (mfumo). Kushikamana na Uislamu kwa maana ya ujumla na kwa ubainifu.

Amesema Allâh (سبحانه وتعالى) : **"Enyi Mlioamini! Ingieni katika hukumu za Uislamu zote."**

Kwahivyo vigawanyo vya Uislamu katika Misingi na Tanzu ni uzushi wa jaahiliyyah ya kisasa na yaliyokusudiwa kwayo ni kuzitatiza fikra za Waislamu na kuwaingiza kwenye vuguvugu la maisha lisilokuwa na msingi wowote katika Dini ya Allâh. Kwa hakika mizizi yake imesambaa kutoka kwa wale ambao walioghadhibikiwa na Allâh, wale wenye kuamini baadhi ya Kitaab na kukadhibisha baadhi nyengine, wale ambao tuloamrishwa kuwakhalifu kwa ujumla na uhalisi. Na kwa hakika umejua ndugu yangu Muislamu kuhusu matunda ya kuwakhalifu Mayahudi na Manaswara ambayo ni kubaki Dini hii kwenye ushindi na nguvu.

Ulinganizi katika Dini ya Allâh (ad-Da'wah) na kuwakumbusha waumini hakusababishi kutengana. Matatizo makubwa yaliyouzonga Ummah wa Ki-Islamu hayatufanyi sisi kuweza kupambanua baina ya uwajibikaji wetu kwa Allâh, wala hayatufanyi sisi kufadhilisha baadhi yake kuliko baadhi nyengine, tukayachukulia baadhi fulani kwa usahali mpaka tukamalizikiya kusema, 'Haya ni mambo madogo-madogo, mambo ya juu-juu, mambo ya kukhitilafiana, au mambo madogo yasiyo na umuhimu ambayo inatulazimu kuwachana nayo na badala yake tuzitilie mkazo juhudi zetu juu ya mambo makubwa ambayo yaliyopelekea kutufarikisha na kuharibu nguvu zetu!.'

Ewe Muislamu, mwenye kuwalingania watu kwa hujja na dalili, umekwisha kujua kutokamana na ahaadeeth hizi tukufu yakwamba kubakia Dini katika hali ya Utukufu kunategemea juu ya kuharakisha kufungua saumu, ambako kumefungamanishwa na kutwa kwa Jua. Basi wale watu na wamche Allâh, wenye kudai yakwamba kufungua saumu wakati wa jua linapokutwa kuwa ni mzozo (fitnah) na kwamba kulingania katika kuihuisha Sunnah hii ni ulinganizi wa upotofu na ujinga na kuwaweka mbali Waislamu na Dini yao. Au kwamba ni ulinganizi usio na thamani na kwamba hapana uwezekano kwa Waislamu kuletwa pamoja na kuungana juu ya haya kwani ni miongoni mwa mas'ala madogo yasiyo na umuhimu tena yenye ikhtilafu, au kwamba ni mambo madogo! (Walaa Hawla walaa Quwwata illa billaah) Na hapana Hila wala Nguvu isipokuwa kwa Allâh.

**Kufungua Saumu Kabla Ya Kuswali Swala Ya Maghrib**

Alikuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) akifungua saumu kabla ya kuswali. Kuharakisha kufungua saumu ni miongoni mwa tabia za Mitume: Kutoka kwa Abud-Dardaa' (رضي الله عنه) *"Mambo matatu ni katika tabia za Utume: Kufanya haraka kufuturu na kuchelewesha kula Daku na kuweka mkono wa kulia juu ya mkono wa kushoto katika swala."*

**Mtu Na Afunguwe Saumu Na Kitu Gani?**

Mtume alikuwa akihimiza kufungua saumu kwa tende na iwapo hazipatikani basi kwa maji na huu ni katika ukamilifu wa huruma yake na pupa lake (صلى الله عليه وسلم) kwa umati wake na kwa kuwanasihi kwake.

Amesema Mola wa walimwengu ambaye aliyemtumiliza Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم) ambaye ni Rehma kwa walimwengu wote: **"Amekufikieni Mtume aliye jinsi moja na nyinyi, yanamuhuzunisha yanayokutaabisheni, anakuhangaikieni. (Na) kwa walioamini ni mpole na Mwenye huruma."**

Kule kukipa kiwiliwili kitu cha tamu wakati ambapo tumbo likiwa tupu inapelekea zaidi kukikubali kitu kile na mwili kufaidika nacho, hususan mwili wenye afya nzuri ambao utaimarishwa na kitu hicho. Ama kuhusu maji, basi mwili huwa kwa kiasi fulani umekauka kutokana na saumu. Kwahiyo iwapo ukavu kama ule utakapoburudishwa kwa maji, basi utapata faida kamili kutokamana na

ENDELEA KATIKA MAKALA YAJAYO